**Endeleza Insha ifuatayo kwa maneno yako mwenyewe na uifanye ya kusisimua.**

Usiku wote sikupata lepe la usingizi. Niliwaza na kuwazua namna siku ambayo ilifuatia ingekuwa ..................................................................................................................

# JARIBIO LA MTIHANI

D003 **DARASA LA NANE - MWAKA 2022** **[8]**

## KISWAHILI : LUGHA

**Muda: Saa 1 Dak. 40**

**SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI**

1. Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 50.
2. Katika karatasi ya majibu hakikisha umeandika:-
   (i) Jina lako (ii) Jina la shule yako

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 hadi 15. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kwa yale uliyopewa.**

____1____ shauri linaloridhisha kama kujua kuwa____2____katika hatari ya kuangamizwa na virusi ____3____ Corona. Aghalabu____4____watu____5____ wenzao wanaohitaji kwenda kwenye vituo vya kupimwa kwa kuwaambia ____6____ wakaambukizwa uwele ule kule. Wenye kuambiwa huzidi ____7____ aushi yao na mwishowe hukosa kuenda kupimwa. Hali____8____ huwafanya kuvamiwa na woga wa____9____.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. Hazipo | B. Hampo | C. Haipo | D. Halipo |
| 2. | A. hayupo | B. hupo | C. haupo | D. hauko |
| 3. | A. mwa | B. vya | C. za | D. la |
| 4. | A. mtasikia | B. tutawasikia | C. utawasikia | D. watawasikia |
| 5. | A. wakitamanisha | B. wakiwatamauka | C. wakitamaukwa | D. wakiwatamausha |
| 6. | A. huenda | B. huwezekana | C. lakini | D. pengine |
| 7. | A. kugofia | B. kuogofya | C. kuhofia | D. kuogopana |
| 8. | A. hii | B. hizo | C. hizi | D. hiyo |
| 9. | A. mwewe | B. kunguru | C. njiwa | D. panzi |

Vifo vingi nchini mwetu____10____na ajali. Dereva na abiria____11____ sheria na kanuni za barabarani. Wanafunzi na____12____kwa jumla wanastahili kupata mafunzo ya____13____na njia nyinginezo za kinga. Matumizi ya vifaa kama____14____za mikononi,pamba, bendeji na____15____, yajulikane na wote ili tusipoteze mioyo ovyo.


| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 10. | A. hutokana | B. hutoka | C. hutoroka | D. kutokana |
| 11. | A. hupuza | B. huzuia | C. huzuilia | D. hupuuza |
| 12. | A. uma | B. umma | C. umaa | D. umati |
| 13. | A. utabibu | B. dharura | C. huduma ya kwanza | D. uuguzi |
| 14. | A. soksi | B. glavu | C. kaptura | D. pete |
| 15. | A. mengineyo | B. zinginezo | C. vinginevyo | D. mingineyo |

**Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo**

16. **Ni nini wingi wa sentensi ifuatayo;**
    Uwele huo ulisababisha kifo cha adinasi wengi.
    A. Mawele hayo yalisababisha vifo vya adinasi wengi.
    B. Ndwele hizo zilisababisha vifo vya adinasi wengi.
    C. Uwele huo ulisababisha vifo vya maadinasi wengi.
    D. Ndwele hizo zilisababisha vifo vya maadinasi wengi.

17. **Chagua sentensi iliyotumia nomino ya makundi**
    A. Bibi yangu amefikisha kame moja hivi majuzi.
    B. Wanasoka wa timu ya shule yetu ni hodari.
    C. Nifikiriapo marehemu baba, mawazo hunisonga.
    D. Mji mkuu wa Kampala umevamiwa na nzige.

18. Ni pembe tatu ngapi zilizopo katika umbo hili?



A. 11
B. 10
C. 9
D. 13

19. **Andika sentensi hii katika usemi wa taarifa**
    Kadogo aliniambia, "Ninataka kununua shamba la mananasi."
    A. Kadogo alisema kuwa nitatanunua shamba la mananasi.
    B. Kadogo aliniambia kuwa alitaka kununua shamba la mananasi.

C. Kadogo alisema kuwa alinunua shamba la mananasi.
D. Kadogo alisema kuwa anataka kununua shamba la mananasi.

**20. Tambua matumizi ya "po" katika sentensi ifuatayo.**
Wakenya walipomchagua rais, alishika hatamu za uongozi.
A. ya masharti B. ya mahali
C. ya amri D. ya wakati

**21. Bainisha maneno yaliyopigwa mstari**
Chungu hiki **cheusi** ni **changu.**
A. kivumishi, kielezi B. Kiarifa, kimilikishi
C. Kiwakilishi, kimilikishi D. Kivumishi, kiashiria

22. Tumia kiunganishi kifaacho kuunganisha sentensi hizi;
Mwai hapendi madondo. Mwai hapendi muhogo.
A. Mwai hapendi madondo wala muhogo.
B. Mwai hapendi madondo na muhogo.
C. Mwai hapendi madondo bali muhogo.
D. Mwai hapendi madondo pia muhogo.

**23. Chagua kundi la vihusishi pekee**
A. chini ya, mkabala na, kusini mwa, nyuma ya
B. jeusi, tamu, bovu, bora
C. fauka ya, mbali na, bila, licha ya
D. Ala! Afanalek! Lahaula! Lo!

24. Chagua vazi la kike linalovaliwa kuanzia kiunoni na kuishia magotini.
A. shimizi B. gaguro C. kanchiri D. kaptura

25. Mhandisi ni ___________
A. aliye na ujuzi wa kuganga viungo vya mwili
B. mwenye ujuzi wa kufua vitu vya madini ya thamani
C. mwenye ujuzi wa kuandika vitabu na majarida
D. mwenye ujuzi wa kuunda mitambo, madaraja na majengo

**26. Kanusha sentensi ifuatayo**
**Kujali kwake kumemsaidia**
A. Kutojali kwake kumemsaidia.
B. Kutojali kwake hakutamsaidia.
C. Kutojali kwake hakujamsaidia
D. Kutojali kwake hakungemsaidia.

**27. Chagua kiambishi kifaacho kujaza pengo**
Sukari_____ ke_____ limwagwa chini.
A. za, zi B. cha, ki C. ya, i D. za, li

**28. Ni nini ukubwa wa;**
Kufuli lake limepotea.
A. kufuli lake limepotea.
B. makufuli yake yamepotea.
C. jikufuli zake zimepotea.
D. jikufuli lake limepotea.

29. Methali nyingine ambayo inaweza kutumiwa badala ya "Ngoja ngoja huumiza matumbo." ni __________
A. Chelewa chelewa utamkuta mwana si wako
B. Pole pole za kombe humdikisha mbali
C. Haraka haraka haina baraka
D. Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe

**30. Chagua sentensi iliyo na "ki" ya kielezi**
A. Tukikosana sana tutachosha bongo.
B. Alifanya kazi hiyo kivoloya.
C. Kile kilichopotea ni chake.
D. Tulikuwa tukiimba alipoingia kanisani.

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 hadi 40**

Samaha aliketi kitako jukwaani akiwa pamoja na wageni mashuhuri walioalikwa katika shule ya upili ya wasichana ya Mwelekeo. Shule hii ilikuwa ya kipekee iliyokuwa imejengwa hivi majuzi kutokana na ufadhili wa Samaha na rafiki zake.

Samaha aliwatupia jicho wanafunzi waliokuwa wamefurika furifuri kisha akajisemeakimoyomoyo, "Wanagenzi hawa wana bahati ya mtende. Wangefahamu waliopitia watoto wasichana wa zama zetu, katu wasingelaza damu masomoni. Wangetambua bidii walizotia dada zao na kujenga shule hii, wangewaiga na kuwa na hamu zaidi ya kutaka kubukua matopa ya vitabu. Nitumie mbinu na lugha gani kuwahamasisha kuhusu umuhimu wa elimu?"

Mwandani wa Samaha alipogundua kuwa Samaha alikuwa kazama katika lindi la fikira, alimgutusha. "Samaha, mawazo mengi, kuna nini? Samaha alishtuka na kufuta michirizi ya machozi iliyokuwa imejichora mashavuni pake. Kumbukumbu za yale aliyoyapitia angali msichana zilimvaa akilini. "Aaah! Ya kale hayanuki. Hakuna haja ya kuwazia yaliyopita. Sasa nitaganga yajayo," Samaha alisema. Hotuba mbalimbali zilitolewa za kusifu Samaha na rafiki zake kwa kujinyima na kujitolea kuimarisha kiwango cha elimu ya wasichana katika jamii ile.

Samaha alikumbuka tena alivyosoma kwa shida licha ya kuwa wazazi wake walikuwa walalaheri. Alikumbuka alivyonyimwa nafasi ya kujiunga na shule ya upili licha ya kufaulu katika mtihani wake wa darasa la nane. Tamaduni na misimamo mikali dhidi ya elimu kwa wasichana viliwafanya wanajamii kutothamini elimu ya wasichana. Waliamini kuwa kusomesha msichana ni kupoteza mali. Wavyele wa Samaha walikiri na kuafikiana na tamaduni hizo potovu. Waliamua na kuoza Samaha kwa shaibu mmoja.

Lo! Samaha bila shaka aliridhia uamuzi huo shingo upande. Alikumbuka jinsi uhusiano ule haukuwa wa ndoa bali doa. Mapingo, matusi, madharau, vitisho vilisheheni ndoa hiyo. Vicheko na madhari ya wanajamii yalizidi pale ambapo ilibainika kuwa amechelewa kupata mbeleko. Mambo yalipozidi unga na kumfika kooni, alikata kauli na kusema hata ikiwa watasema mwacha mila ni mtumwa, wacha waseme. Aliwaza na kuwazua na kumtembelea mama mmoja aliyeitwa Mkombozi. Mkombozi alikuwa mwanzilishi wa shule ya watu wazima. Alimshauri Samaha ajiunge na kituo hicyho ili apate elimu. Samaha alitia shime masomoni na kunakili chochote alichokisoma akilini mwake. Aliamini kuwa elimu haina umri wala mwisho. Alijifunga masombo na akasoma hadi chuo kikuu.

Alifaulu katika masomo yake ya chuo kikuu na kurudi kwao. Huko, alipata ajira iliyomwezesha kukidhi mahitaji yake pamoja na ya wazazi wake. Aidha, alianzisha miradi mbalimbali kijiji. Miradi hiyo ilikuwa na lengo hasa la kuinua na kuimarisha maisha na heshima ya mtoto msichana kijijini humo. Ufanisi wa Samaha uliwakosesha amani waliomdhulumu mtoto msichana hapo awali. Walimsingizia hili na lile lakini mbinu zao hazikufanya lolote kuzima kiu ya Samaha ya kujiendeleza. Aliwapuuzilia mbali akisema kuwa katu jua haliwezi kuzuiwa kwa ungo.

Baada ya takribani miaka minne, bwana ya Samaha alimuomba msamaha. Samaha alikubali na kurudiana naye. Aliwasamehe wote waliomdhulumu. Aliwaona kuwa walioongozwa na tamaduni na itikadi zilizopitwa na wakati. Aliwafahamisha wanakijiji umuhimu wa kutobagua mwanamke. Aliwafunza ubora wa mtoto wa kike kupata elimu. Mafunzo ya Samaha yalikumbatiwa na wanakijiji. Waliwasomesha wana wa jinsia zote. Baada ya muda mchache, kijiji cha Mwelekeo kilipiga hatua kubwa katika ufanisi. Maendeleo yalijitokeza, si shule kujengwa, si hospitali si miundo msingi. Kilichokuwa kikizama kikaokolewa.

Sifa za Samaha zilitanda pande zote Mwelekeo. Hata vijiji jirani vilisikia sifa hizo. Akawa wa kupigiwa mfano. Bidii yake ya kuonya jamii dhidi ya mila potovu ikazaa matunda. Samaha akabaki kuwa kielelezo bora kwa kila mja, wazee kwa vijana.

31. Wanafunzi wa shule ya upili ya mwelekeo walikuwa na bahati ya mtende kwa kuwa ________
   A. shule yao ilijengwa kwa ufadhili wa wasamaria wema
   B. walipata nafasi bora ya kupata elimu
   C. walibaguliwa kimasomo kama hapo awali
   D. shule yao ilikuwa ya mwanza kujengwa kijijini

32. Ni kwa nini michirizi ya machozi ilitiririka mashavuni pake Samaha?
   A. Alikumbuka mateso aliyokuwa anayapitia wakati huo
   B. Alikumbuka alivyojitahidi na kutoroka ndoa
   C. Alikumbuka mafanikio aliyokuwa amepata wakati huo
   D. Alikumbuka mateso aliyopata angali msichana mdogo

33. Kulingana na taarifa, ni haki gani ya mtoto msichana iliyokiukwa na wanakijiji?
   A. Haki ya kumpa mwana msichana elimu
   B. Haki ya kumuoza mtoto msichana mapema
   C. Haki ya kutompa mwana msichana heshima
   D. Haki ya kumpa msichana hiari ya kujichagulia atakacho

34. Je mwandishi ana msimamo upi kuhusu elimu?
   A. Elimu hupatikana na mtu yeyote na mahali popote
   B. Elimu kwa msichana ni bora zaidi kuliko kwa mvulana
   C. Elimu haina umri wala mwisho
   D. Elimu bora hupatikana baada ya kujiunga na chuo kikuu

35. Ni sifa zipi ungeipa jamii ya Samaha kulingana na habari hii?
   A. Tamaa, uongo, woga, chuki
   B. Ubinafsi, upendo, maridhiano, ulafi
   C. Ulaghai, usalama, chuki, urafiki
   D. Ukatili, ubaguzi, msamaha, umoja

36. Kijiji cha Mwelekeo kilizorota na kurudi nyuma kimaendeleo kwa sababu ya
   A. kutowaelimisha wanawake
   B. kuwaoza wasichana wangali wachanga
   C. kupuuza mchango a vijana katika ufanisi wa jamii
   D. kuthamini na kufuata itikadi na mila potovu

37. Elimu ya Samaha iliwawezesha raia wa Mwelekeo kufanya haya yote ila __________
   A. kustawisha kijiji na kuboresha huduma za afya
   B. kutilia mkazo masomo ya msichana kuliko ya mvulana
   C. Kupanua miundo misingi katika kijiji chao
   D. Kutupa mila na tamaduni potovu katika kaburi la sahau

38. "Ilibainika kuwa amechelewa kupata mbeleko" Maneno haya yametumika katika kifungu kumaanisha
   A. Samaha hakumtuza bwana wake kama walivyotarajia raia
   B. Samaha alichelewa kupata masomo
   C. Samaha alichelewa kuwa mjamzito na kupata mtoto
   D. Samaha hakutaka kuwa mjamzito mapema

39. Ni methali gani inayoafikiana na juhudi alizofanya Samaha katika kijiji cha Mwelekeo?
   A. Mkulima ni mmoja walaji ni wengi.
   B. Mwende tezi na omo marejeo ni ngamani.
   B. Mchagua jembe si mkulima.
   D. Mstahimilivu hula mbivu.

40. Chagua kichwa mwafaka zaidi kwa kifungu hiki.
   A. Umuhimu wa kuwa na marafiki
   B. Msichana ni ufanisi wa jamii
   C. Umuhimu wa elimu kwa wote
   D. Ufadhili nguzo muhimu

**<u>Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 41 hadi 50</u>**

Uchukuzi katika mataifa mengi ya Afrika ni taabu sana. Wengi wa waja hupiga milundi kwa muda mrefu kwa kuukosa usafiri wa haraka. Wengine hupanda hata ngamia ili wapige hatua. Punda hutumiwa mara kwa mara kusafirisha mizigo. Waliobahatika na kununua magari, hugharamika mara si haba kwa ukarabati wa magari hayo. Magari mengi ya aina hiyo huwa tu ni ya kubebewa <u>jeki, nyundo na spana</u> kila wakati. Hali hii inasababishwa hasa na barabara ambazo hazijatiwa lami. Na zile zilizo na lami basi lami hiyo ni bandia. Mashimo na vidimbwi barabarani huharibu magurudumu na hata injini za magari yenyewe. Halikadhalika, ukata katika jamii unachangia pakubwa uhaba wa magari mazuri na hata ubovu wa hayo machache. Hii ni kwa sababu watu hawana senti za kununulia vipuri vifaavyo au kujinunulia magari mapya.

Kunao wanaotumia baiskeli kwa usafiri wao kwa sababu zina nafuu ukilinganisha na magari. Iwapo ni nafuu kwa fedha, lakini haziwezi kubeba mizigo mingi na mizito. Ni wachache sana wanaotumia meli na eropleni. Magari moshi hutumiwa kwa wingi kwa kuwa hubeba watu na vitu kwa wingi. Ukarabati wa reli injini na mabehewa ya magari haya una gharama kali. Jambo hili limesababisha kuongezeka kwa nauli katika miaka ya hivi karibuni. Wasafiri wengi wameshindwa kuulipia usafiri huo. Wengi hasa vijana, hudandia mabogi na mabehewa ili tu wakwepe kulipa nauli. Hulka hii si tu tishio kwa shirika la reli bali pia hatari kwa wasafiri. Wachache wa wanaodandia huporomoka na kuvunjika viungo, jambo ambalo huongeza idadi ya walemavu nchini. Daladala na mabasi ni aina ya uchukuzi ambao ni maarufu humu nchini. Uchukuzi huu umewafaa wengi kwa miaka na dahari, hasa wale wa kipato cha chini na wale wa wastani. Kinachowaudhi wasafiri sana ni ukosefu wa uangalifu na kutodhibiti mambo fulani katika sekta hii. Kujaza abiria garini kama makopa, tabia mbi za dereva na utingo, kutodhibiti mwendo wa magari hayo ni baadhi tu vya mambo yanayowakera wasafiri na kuufanya uchukuzi huu kupakwa tope. Zaidi ya hayo, imekuwa ni shida kuzidhibiti tabia za wale wapendao kurambishwa asali katika sekta hii.

Siku chache zilizopita, waziri wa uchukuzi na miundomsingi alibuni mikakati ya kusafisha maovu katika sekta hii. Sheria ziliundwa za kuhakisha kwamba wenye magari wanaweka vidhibiti mwendo abiria kufunga mikanda ya usalama, utingo na dereva kuvaa sare na kutundika picha zao magarini pia na kutobeba abiria kupita kiasi. Wale wasioweza kutimiza masharti hayo, magari yao yaliwekwa pembeni. "Si hoja hata kama itabidi tutembee kwa miguu kwa muda ni sawa, mradi tupate suluhu la kudumu." Abiria walisikika wakisema.

Masharti haya yameleta heshima na utaratibu katika sekta ya uchukuzi. Ajali za barabarani zimepungua kwa kiasi kikubwa mno. Utingo na madereva wamefahamu kuwa heshima si utumwa.

---

**41.** Ni aina zipi za usafiri ambazo zimetajwa na mwandishi?
A. miguu, garimoshi, baiskeli
B. baiskeli, pikipiki, ndege
C. wanyama, miguu, udandiaji
D. pikipiki, udandiaji, garimoshi

**42.** Kulingana na taarifa hii,ni nini sababu kuu ya wasafiri kudandia gari moshi?
A. Usafiri wa magari na ndege ni ghali
B. Usafiri wa garimoshi ni wa ustaarabu
C. Wanakwepa kulipa nauli
D. Usafiri wa gari moshi huwa nafuu kwa kawaida

**43.** Kulingana na habari, ni chombo kipi cha usafiri kinachotumiwa na waja wengi?
A. matatu B. eropleni
C. baiskeli D. gari moshi

**44.** Ni yapi kati ya haya yanayochangia kuzorota kwa uchukuzi?
A. Upungufu wa magari, ukwepaji kulipa nauli, lami mbovu
B. Mabonde barabarani, uendeshaji mbaya wa magari, umaskini
C. Ukosefu wa lami, kudandia gari moshi, bei ghali ya baiskeli
D. Ukosefu a vidhibiti, ukata, njia mbovu za uchukuzi

**45.** Magari yanayobebewa spana na jeki kila wakati ni ya aina gani?
A. Mapya B. Mabovu
C. Makubwa D. Mepesi

**46.** Kwa mujibu wa kifungu, kujivunjia viungo kunamaanisha
A. kuvunjavunja viungo kwa kusudi
B. kuvunja viungo kwa sababu fulani
C. kujisababishia kuvunjika kwa viungo
D. kuvunja viungo vyako mwenyewe

**47.** Unafikiri suluhisho mwafaka la usafiri wa barabarani kulingana na kifungu ni
A. kuwashika na kuwashtaki wasiofuata masharti
B. kupunguza idadi ya magari barabarani
C. kuwaadhibu wanaopenda kurambishwa asali
D. kuwazungumzia wasafiri, polisi na wenye vyombo vya uchukuzi

**48.** Abiria walisikika wakisema, "Si hoja, hata kama itabidi tutembee kwa miguu" kwa sababu ___________
A. walikuwa wamechoka na nauli ghali ya gari moshi
B. walikuwa wameudhika na shughuli zote za uchukuzi
C. walitaka vidhibiti mwendo na mikanda ya usalama
D. walichoka na usafiri wa barabara

**49.** Ni nini maana ya "wapendao kurambishwa asali"
A. Wapendao hongo.
B. Wapendao vya bwerere.
C. Wapendao anasa.
D. Wapendao kulamba sana.

**50.** Masharti yaliyowekwa katika sekta ya usafiri hivi majuzi yamesabisha haya yote ila __________
A. Utingo na madereva sasa wanaheshimu abiria.
B. Ajali za barabarani zimepungua.
C. Kumekuwa na ongezeko la magari ya uchukuzi barabarani.
D. Kuna utaratibu katika sekta ya uchukuzi.